

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MJI WA TARIME  
SHULE YA SEKONDARI REBU**

SHULE YA SEKONDARI – REBU  
S. L.P 225  
**TARIME.**

**04/12/2020**

**Kumb. Na: HMT/RSS/AD/2021**

Jina la mwanafunzi \_\_\_\_\_

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI REBU ILIYOKO WILAYA YA TARIME  
MKOA WA MARA MWAKA 2021**

**1: 0 UTANGULIZI:**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari – Rebu mwaka 2021

Shule ya Sekondari – Rebu ipo umbali wa km 1.5 Mashariki mwa Mji wa Tarime.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **19/01/2021** (ndani ya siku saba).

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE**

**A. WASICHANA**

- (i) Shati mbili mikono mifupi zisibane kuonyesha nguo za ndani, ziwe na mfuko mmoja tu upande wa kushoto wenye nembo ya shule (utaratibu wa kupata nembo ya shule utafahamishwa siku ya kuripoti). Ziwe ndefu na zenye kuchomekeka vizuri.
- (ii) Sketi mbili nyeusi kitambaa cha sutiyenye marinda inchi moja na nusu, mkanda wa sketi inchi mbili, zitakuwa na tepe/fito mbili nyeupe mbele kuanzia kiunoni hadi chini. Sketi inatakiwa iwe ndefu kufika karibu na enka (kifundo cha mguu).
- (iii) Viatu vya ngozi vyenye visigino vifupi, vinavyofunika miguu, na vyenye kufungwa kwa kamba
- (iv) Soksi nyeupe ndefu aina ya stockings, zisizo na mapambo ya aina yoyote.
- (v) T-shirt ya shule mikono mifupi yenye nembo ya shule (utaratibu wa kuzipata utafahamishwa siku ya kuripoti)
- (vi) Tainyeusi zenye nembo ya shule (utaratibu wa kuzipata utafahamishwa siku ya kuripoti).

**B. WAVULANA**

- (i) Shati mbili mikono mifupi zisibane kuonyesha nguo za ndani, ziwe na mfuko mmoja tu upande wa kushotowenye nembo ya shule (utaratibu wa kupata nembo ya shule utafahamishwa siku ya kuripoti). Ziwe ndefu na zenye kuchomekeka vizuri.
- (ii) Surali mbili rangi nyeusi zilizoshonwa kwa staha, luksi sita zenye upana wa kutosha, marinda mawili upande wa kushoto na kulia, mkunjo (turn up) sehemu ya miguuni na

mzunguko wa mguu kwa chini usipungue **nchi 18**. Suruali aina ya “**MODO**” hazitakiwi shuleni.

- (iii) Viatu vyangozi vyenye visigino vifupi, vinavyofunika miguu vyenye kufungwa kwa kamba
- (iv) T-shirt ya shule mikono mifupi yenye nembo ya shule (utaratibu wa kuzipata utafahamishwa siku ya kuripoti)
- (v) Tainyeusi zenye nembo ya shule (utaratibu wa kuzipata utafahamishwa siku ya kuripoti)
- (vi) Soksi nyeupe zisizo na mapambo ya aina yoyote na mkanda mweusi.
- (vii) Passport size moja ya Mzazi au Mlezi halali

**NB. Ukija na sare ya shule iliyoshonwa bila kufuata maelekezo hapo juu hutapokelewa’**

## **2.2 MAHITAJI MENGINE**

### **KWA WASICHANA NA WAVULANA**

- (i) Uwe na mfuko wa kuhifadhia madaftari yako (school bag). Mifuko yenye picha za wasanii hairuhusiwi.
- (ii) Sweta la rangi ya bluu yenye shingo la V
- (iii) Mapambo ya aina yoyote hayaruhusiwi shuleni kama vile mikufu, hereni, rangi za kucha na midomo kupaka lipstick, wanja n.k.
- (iv) Mkebe wa hesabu (mathematical set), rula, kalamu, Dictionary.
- (v) Madaftari makubwa (counter books) kumi na mbili (12) na madaftari madogo (msomi) matano
- (vi) Nguo za michezo (track suit) rangi ya bluu nyeusi (dark blue) na raba za michezo.
- (vii) Nywele lazima ziwe fupi, kusuka hairuhusiwi.

## **3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule itaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshajiElimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- (c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- (d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
- (e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- (f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- (g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- (h) Kutunza mali za UMMA

### **3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocain, mirungi, kubeli nk
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya UMMA
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito, kupata mimba au kusababisha ujauzito
9. Kutoa mimba
10. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa watu au shule
11. Kukataa adhabu kwa makusudi
12. Kuwa na simu ya mkononi

### **4: 0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

- (a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- (c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- (d) Nakala ya cheti cha kuzaliwa

**Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**Nakutakia maandalizi mema**

.....

**NELSON D MAKORO**

**MKUU WA SHULE**

**4.1. FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA  
KUTII SHERIA NA KANUNI ZA SHULE NA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO , FUJO NA  
MAKOSA YA JINAI**

Mimi \_\_\_\_\_ (jina la mwanafunzi) nakubaliana na maagizo yote yalioelekezwa katika barua ya maelekezo niliyopewa na shule. Naahidi kwamba kwa muda wote nitakaokuwa hapa shuleni nitatii na kuyatekeleza kwa dhati, kinyume chake sijaelimika na kutimiza wajibu wangu. Kwa jinsi hiyo uongozi wa shule utachukua jukumu la kuniondoa na kunisimamisha masomo.

Naahidi pia kuwa nitajielimisha kadri ya uwezo wangu wote, na kwamba nitaitumia elimu kwa manufaaya wananchi wenzangu wote.

Saini.....

Jina la mwanafunzi.....

Tarehe.....

**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**Tafadhali sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi kwa uangalifu na taarifa ziwe sahihi.**

1. Jina la mwanafunzi.....  
Kijiji/ Mtaa anakoishi..... Kata.....  
Wilaya..... Mkoa.....
2. Majina ya wazazi/walezi
  - i. Jina la baba mzazi/mlezi.....  
Kijiji/mtaa anakoishi.....Kata .....
  - Wilaya..... Mkoa.....  
Kazi yake.....Simu Na.....
  - ii. Jina la mama mzazi/mlezi.....  
Kijiji/mtaa anakoishi ..... Kata .....
  - Wilaya.....Mkoa.....  
Kazi yake..... Simu Na .....
3. Ndugu wa karibu wa mwanafunzi  
Jina lake .....  
Uhusiano.....  
Kijiji /Mtaa anakoishi .....Kata.....  
Wilaya..... Mkoa .....
- Simu Na. ....
4. Dini / dhehebu analosali mf. RC, SDA, UISLAMU nk, .....

#### 4.2. FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.

Mimi .....(jina la mzazi/mlezi) naahidi kushirikiana na walimu katika malezi ya mwanangu akiwa shule na hata nje ya shule. Na kwamba ni wajibu wangu kama mzazi / mlezi kumhimiza mwanangu asome kwa bidii na afuate sheria na taratibu zote za shule.

Pia nitalipa michango ya shule itakayokubaliwa na kupitishwa na wazazi katika muda uliopangwa na kwamba kila mwisho wa muhula nitamtaka mwanangu anipe taarifa ya maendeleo yake kitaaluma na tabia kwa ujumla na kurudisha ripoti shuleni.

Saini ya mzazi/mlezi .....

Jina la mzazi/mlezi.....

Tarehe.....

Endapo sitapatikana kwa sababu yoyote ile naomba mawasiliano yafanyike kwa walezi wafuatao:-

1. Jina .....  
Uhusiano .....  
Kijiji/Mtaa .....  
Kata ..... Wilaya .....  
Mkoa ..... Namba ya simu.....

2. Jina .....  
Uhusiano .....  
Kijiji/Mtaa .....  
Kata ..... Wilaya .....  
Mkoa ..... Namba ya simu.....

3. Jina .....  
Uhusiano .....  
Kijiji/Mtaa .....  
Kata ..... Wilaya .....  
Mkoa ..... Namba ya simu.....

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
THE PRESIDENT'S OFFICE  
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT  
FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

---

To be completed by a medical officer in respect of all form one students.

Pupil's name .....

Age .....

Blood count (Red and White) .....

Urinalysis .....

Syphilis Test .....

T.B Test .....

Eye Test .....

Ear Test .....

Chest .....

Spleen .....

Abdomen .....

ADDITION INFORMATION . eg Physical defects of impairment (s) infections, chronic or family diseases, etc.

.....  
.....  
.....

I certify that the above is fit to pursue further as stated above.

Signature .....

Designation .....

Station .....

Date .....